

Hakuna maendeleo endelevu bila nishati endelevu

Na Albano Midelo

MOJA ya miradi ambayo inatekelezwa na Shirika la uhifadhi mazingira la dunia (WWF) ni kuhamasisha jamii kuondokana na matumizi ya nishati isiyokuwa endelevu na kujikita katika nishati endelevu (Renewable energy).



Mtaalam wa Nishati, Gesi na Mafuta wa Shirika la kimataifa la uhifadhi endelevu la WWF Mjiolojia Roy Namgera anaeleza kuna aina mbili za nishati ambazo ni nishati endelevu na nishati ambazo sio endelevu.

Anazitaja baadhi ya nishati ambazo zinaingia katika kundi la nishati endelevu kuwa ni nishati upepo, nishati jua, joto ardhi, nishati ya umeme, nishati ya mawimbi ya bahari, nishati ya mawimbi ya maji, nishati ya nguvu ya maji, nishati ya mabaki ya mimea, nishati ya vinyesi vya wanyama na nishati nyingine.

Anazitaja nishati ambazo zinaingia kwenye kundi la nishati ambazo sio endelevu kuwa nishati ya nguvu za nuklia, nishati za gesi, makaa

ya mawe,kuni,mkaa, mafuta na nishati nyingine ambazo zinachimbwa na kumalizika hivyo sio endelevu.



Kulingana na Mjiolojio huyo nishati zote ambazo sio endelevu zimebainika zina madhara kiafya na kimazingira,hivyo nchi zote duniani zinatakiwa kubadilika katika matumizi ya nishati na kuanza kutumia zaidi nishati endelevu.

Kutokana na umuhimu wa nishati endelevu katika maendeleo na mazingira nchi ya China inatarajia kuongeza uwekezaji wa Dola za Marekani bilioni 361 kwenye sekta ya nishati endelevu katika miaka mitano ijayo na kuifanya nishati hiyo kuwa chanzo kikuu cha ongezeko la nishati na nguvu ya umeme nchini China.

Naibu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Nishati ya China Li Yangzhe amesema, inatarajiwa kuwa matumizi ya nishati endelevu yatafikia asilimia 15 ifikapo mwaka 2020, na asilimia 20 mwaka 2030.

“Kipaumbele kitawekwa katika kuhimiza matumizi ya vyombo vya usafiri vinavyotumia nishati safi, gharama ndogo za nishati endelevu kama vile upepo, kuongeza ufanisi wa matumizi ya nishati

endelevu na kuongeza ubunifu na ushirikiano wa uzalishaji wa kimataifa kwenye sekta ya nishati”, anasisitiza Yangzhe.

Katika hatua nyingine ya kuimarisha matumizi ya nishati endelevu, Umoja wa Mataifa umelenga kutumia zaidi rasilimali za nishati endelevu ikiwemo jua, ili kuzalisha umeme kwa matumizi ya majumbani na shughuli zingine.

Inakairiwa kuwa asilimia 70 ya mahitaji ya umeme duniani yanaweza kutolewa kwa kuvuna nishati ya jua kali linalowaka katika barani Afrika na Bara la Asia.



Rachel Kyte, ni Mwakilishi maalum wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kwa ajili ya nishati endelevu kwa wote, anaamini kuwa nishati ya jua inaweza kuzalisha umeme katika ukanda wa Afrika na hata kwa jamii za nje ya ukanda huo.

Analitaja lengo la Umoja wa Mataifa ni Kuhakikisha wananchi duniani kote wanapata nishati endelevu ya bei nafuu na kwamba nishati endelevu kama ya jua ina umuhimu mkubwa katika maisha ya kila kiumbe duniani.

Umuhimu wa jua umeanza kukubalika zaidi katika kuzalisha nishati na kwamba nishati hiyo imekuwa inatumia teknolojia rahisi kuzalisha umeme kutokana na jua kwa kutumia paneli za jua.

Uchunguzi umebaini kuwa kutumia vyanzo vya nishati ambavyo sio endelevu kama vile mafuta, makaa na gesi asili husababisha uharibifu au uchafuzi wa mazingira.

“Kama chanzo mbadala jua linaweza kuzalisha nishati ambayo ni endelevu n isiyopungua,ni nishati safi ambayo haisababisha uharibifu wa mazingira kwa kutoa gesi wala moshi wala kusababisha mionzi katika hewa”,anasisitiza Roy Namgera Mtaalam wa nishati wa Shirika la WWF.

Amesema matumizi ya nishati ya jua ni jambo linaloweza kuchangia katika kulinda mazingira yetu,na kwamba paneli za jua zinaweza kuwekwa kwa gharama ndogo.

Utafiti umebaini kuwa nchi ya Uturuki ipo katika eneo zuri la kuzalisha umeme kutokana na jua. Hata hivyo Kiasi cha nishati ya jua kinachotumiwa katika nchi hiyo ni kidogo ikilinganishwa na kiasi cha jua kinachoweza kutumiwa.

Iwapo **Uturuki** itaweza kutumia nishati ya jua vyema zaidi basi nchi hii itaweza kuepuka kutegemea nchi za nje kwa ajili ya vyanzo vya nishati kama vile mafuta.

Utafiti umebaini kuwa katika Nchi nyingi za bara **Afrika** hupata mwanga wa jua kwa takriban saa **12** kila siku hali ambayo inadhihirisha kuwa nchi hizo zina fursa kubwa ya kuzalisha nishati endelevu kwa kutumia nishati ya Jua.

Utumiaji wa nishati ya jua unaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa katika kuimarisha uchumi wa nchi hizi na pia kuepusha nchi hizo

kutegemea nchi za nje kwa vyanzo vya nishati au kutumia nishati ambazo sio endelevu.

Ili kuimarisha matumizi ya nishati ya jua inashauriwa Kuongeza idadi ya paneli za jua, Kutumia bateri zinazoweza kuongezwa nguvu kwa kutumia nishati ya jua na Kuongeza matumizi ya jua katika kupasha maji moto.

Nishati ya jua ni nishati isiyopungua, nishati isiyokuwa na madhara yeyote na nishati ya bure hivyo nishati hiyo ni endelevu ambayo ina umuhimu mkubwa katika kuimarisha usafi wa hewa na uchumi wa nchi mbalimbali duniani.

Licha ya nishati ya Jua, nishati endelevu nyingine ni zinazotokana na masalia ya mimea na wanyama ambapo wakazi wa Uganda wanategemea nishati inayotokana na wanyama na mimea.

Tafiti zilizofanywa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) zinaonesha kuwa kuni na mkaa vinachangia asilimia 88 ya matumizi yote ya nishati nchini humo. Umeme na gesi nyingine vinachangia sehemu iliyosalia.

Kuanzishwa kwa utafiti wa mradi wa nishati rafiki na matumizi bora ya nishati mbadala ni njia moja ya kuiwezesha Zanzibar kuwa na vyanzo vyake vya ndani vya nishati.

Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, Tahir Mohammed, amesema mradi huo umejihusisha na utafiti wa kuangalia uwezekano wa kuzalisha umeme kutokana vyanzo vya nishati ya upepo na jua.

Amelitaja lengo ni kupata ufumbuzi wa kuwa na nishati endelevu ambayo itahifadhi mazingira.

Amesema kukamilika kwa utafiti huo kutaisaidia serikali kuweka mazingira wezeshi kisera na kisheria kwa ajili ya kuwezesha nishati rafiki na kutoa elimu ya ufahamu kwa wananchi na sekta binafsi kuhusu nishati mbadala.

Amesema Zanzibar inakosa chanzo muhimu cha nishati ya maporomoko ya maji na badala yake inategemea nishati ya umeme kutoka Tanzania bara.

Amebainisha kuwa, kuharibika kwa mazingira huathiri maisha ya viumbe vingine kama binadamu, wanayama na hata mimea hivyo ni vyema nishati hizo ziwe rafiki na mazingira na vitu vilivyomo.

Omar Saleh Mohammed, Msaidizi Mkuu wa mradi wa nishati rafiki kutoka idara ya nishati na madini, amesema, hivi sasa wamejikita zaidi katika vyanzo vya jua na upepo na utafiti uliofanywa mwaka 2012 ulibainisha vyanzo vingi lakini vilivyopata nafasi ya kwanza ni jua na upepo.

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan amesema kuwa ongezeko la watu katika miji mikubwa kuna changia sana katika uharibifu wa mazingira na matumizi makubwa ya mkaa.

“Dar es Salaam peke yake inakadiriwa kutumia kati ya magunia kati ya 200,000 mpaka 300,000 yenye uzito wa kilo 50 kila moja ya mkaa kwa mwezi na inategemewa itaongezeka zaidi kutokana na kasi ya ongezeko la watu hasa kwenye miji, ”alisema Makamu wa Rais.

Makamu wa Rais amewata Watanzania, kampuni pamoja na Taasisi mbalimbali kuungana na Serikali kubadilisha jamii yetu kuanza kutumia nishati ya majani kwa namna ya mkaa na kuni kama vyanzo mbadala vya nishati endelevu.



Makamu wa Rais amewataka Wananchi wabadilike badala ya kutumia mkaa ambao unasababisha ukataji mkubwa wa miti ni vyema kuanza kutumia nishati mbadala.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, January Makamba alisema kutokana na uhitaji na umuhimu wa kutunza mazingira Serikali, Wadau wa Maendeleo, Taasisi mbali mbali, Sekta Binafsi na Watungaji wa Sera kutafakari kwa pamoja na kuja na majawabu yatakayosaidia katika utunzaji wa mazingira na kuilinda miti.

Balozi wa Sweden nchini Tanzania, Katarina Rangnitt amesema tangu mwaka 1972 changamoto za uharibifu wa mazingira hazikuwa za Kikanda tu bali ni kwa dunia nzima hivyo hili jambo linahitaji ushiriki wa Dunia nzima katika kupambana na uharibifu wa mazingira kwa kutumia nishati endelevu.

Mwandishi wa makala haya ni Albano Midelo

Mawasiliano yake albano.midelo@gmail.com,simu 0784765917